


Nozibele na nywele tatu



Tessa Welch

Wiehan de Jager

Matteo E. Mwita

Kiswahili

Level 3



Storybooks Zambia


[global-asp.github.io/storybooks-zambia](https://github.io/storybooks-zambia)

Nozibele na nywele tatu

Written by: Tessa Welch

Illustrated by: Wiehan de Jager
Translated by: Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Zambia in an effort to provide children's stories in Zambia's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.

<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>





Hapo zamani za kale, wasichana watatu walienda kukusanya kuni.

Mbwa akagundua kuwa Nozibele
amemkimbia. Kwa hiyo akakimbia kuelekea
kijijini. Kaka zake Nozibele walikuwa
wakimsubiri na fimbo. Mbwa alipowaona
akageuka na kukimbia, na hajawahi
kuonekana tena.



Ilikuwa ni siku yenye jua kali na wakamua
kwenda mtoni kuogelea. Wakaogelea huku
wakicheza na kurushiana maji.





Ghafla waligundua kuwa muda umekwenda. Wakaharakisha kurudi nyumbani.




Mbwa aliporudi akaanza kumtafuta Nozibele. "Nozibele, uko wapi?" akapiga kelele. "Niko hapa, chini ya kitanda," unywele wa kwanza ukajibu. "Nipo hapa nyuma ya mlango," unywele wa pili ukajibu. "Niko hapa kwenye uzio," unywele wa tatu ukajibu.



Walipokuwa wanakaribia kufika nyumbani,
 Nozibele akajishika shingoni. Alikuwa
 amesahau shanga zake! "Tafadhali
 turudini!" aliwasihi rafiki zake. Lakini rafiki
 zake wakasema tumechelewa.



Mara bada tu ya mbwa kuondoka,
 Nozibele akanyofoa nywele tatu kutoka
 kwenye kichwa chake. Akaweka unywele
 mmoja chini ya kitanda, mmoja nyuma ya
 mlango, na mwingine akauweka kwenye
 uzio wa nyumba. Halafu, akakimbia
 kuelekea nyumbani kwa nguvu zote.




Kwa hiyo Nozibele akarudi mwenyewe mtoni. Akapata shanga zake na akakimbia kurudi nyumbani. Lakini akapotea gizani.



Akawa kila siku anampikia, anamfulia na kumfagilia mbwa. Siku moja mbwa akasema, “Nozibele, leo naenda kuwatembelea rafiki zangu. Fagia nyumba, pika chakula na osha vitu vyangu kabla sijarudi.”



kwa mbali akaona mwanga unatoka
kwenye nyumba. Akakimbilia kwenye
nyumba na kugonga mlango.



Mbwa akamwambia, "Nitandikie kitanda!"
Nozibele akajibu, "Sijawahi kumtandikia
mbwa kitanda." "Tandika kitanda, la siyo
nitakung'ata!" mbwa akasema. Nozibele
akatandika kitanda.



Akastaajabu kumwona mbwa akifungua mlango na akasema, “Unataka nini?” “Nimepotea na ninatafuta sehemu ya kulala,” akasema Nozibele. “Ingia ndani, la sivyo nitakung’ata!” mbwa akamwambia. Nozibele akaingia ndani.



Mbwa akamwambia, “Nipikie!” “Sijawahi kumpikia mbwa,” akajibu. “Pika, la sivyo nitakung’ata!” mbwa akasema. Nozibele akampikia mbwa chakula.